# KCPE 2004

**Maswali 1 mpaka 15.**

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Kristina alijiangalia tena kiooni. Akauona uso wake uliosawijika na kujaa mabaka ya kila aina. __1__ vimbe lililosimama kwa __2__ kwenye paji la uso wake kana kwamba lilitaka kumkumbusha jambo ambalo daima alitaka __3__. Kwa mbali akaanza kujiwa na kumbukizi. Akayakunjua maisha yake ya __4__. Akavuta fikira tena na kuona jinsi __5__ mjini na kuingilia anasa za mji bila tahadhari. Akajiangalia tena asiweze kuamini macho yake, kakonda ghaya ya kukonda, kabaki __6__ Machozi __7__ njia mbili mbili. Akalia kwa kite na imani, akililia ujana wake, akililia maisha yake; __8__ angalijua! "Lakini, ah!" __9__. "Ya kumwagika yamemwagika. __10__. Niliufaidi uhondo wa mji, kwa nini nijute? Hawakusema wasemao kuwa __11__?"

1. A. Akalitazama B. Akavitazama C. Akazitazama D. Akaitazama
2. A. imara B. dharau C. thabiti D. dhahiri
3. A. kujitambulisha B. kujiondoa C. kujisahaulisha D. kujiandaa
4. A. baadaye B. usoni C. kisasa D. kisogoni
5. A. alivyojihamisha B. alivyojichomoa C. alivyojitoma D. alivyojinasua
6. A. pandikizi la mtu B. gofu la mtu C. fuvu la mtu D. nofu la mtu
7. A. yakambubujika B. yakamlengalenga C. yakammwagika D. yakamsonga
8. A. sembuse B. maadamu C. minghairi D. laiti
9. A. Akagusa moyo B. Akapiga moyo C. Akajipa moyo D. Akasuta moyo
10. A. Haidhuru B. Haizuru C. Haiaminiki D. Haieleweki
11. A. uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti B. gae huwa chombo wakatiwe C. majuto ni mjukuu D. nzi kufa juu ya kidonda si hasara

Dhana inayotolewa kwenye misahafu kuwa mwanamke katolewa kutoka ubavuni mwa mwanamume imechangia pakubwa __12__ mwana wa kike. Katika jamii nyingi nchini mwanamke alichukuliwa kama kitegauchumi kwani mara tu __13__ alitafutiwa mume aliyemwoa na kutoa mahari chungu nzima. Msichana daima hufunzwa kufanya kazi zisizohitaji nguvu nyingi ati __14__ ni za kiume. Katika baadhi ya jamii ilikuwa ni __15__ kwa mwanamke kula vyakula vyenye chembechembe muhimu za kuhifadhi afya kama vile ini. Hivi viliachiwa wanaume.

12. A. kumtwaza B. kumtweza C. kumheshimu D. kumstahi
13. A. alipochuchuka B. alipochachamaa C. alipodumaa D. alipokopoka
14. A. kazi za kijungu jiko B. kazi za shokoa C. kazi za sulubu D. kazi za ujima
15. A. mila B. mwiko C. halali D. desturi

*Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.*

**16.** Ni methali ipi inayoafikiana na maelezo kuwa: Haifai kuwadharau watu waliokusaidia hapo awali, huenda ukahitaji msaada wao tena?
A. Ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno
B. Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi
C. Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani
D. Usitukane wakunga na uzazi ungalipo

**17.** Chagua wingi wa sentensi: Hukujua kuwa ningekutembelea?
A. Hawakujua kuwa tungewatembelea?
B. Hamkujua kuwa tungewatembelea?
C. Hamkujua kuwa ningewatembelea?
D. Hawakujua kuwa ningewatembelea?

**18.** "Shinda" ni kuwa wa kwanza katika jambo. Maana nyingine ni:
A. Bila kujaa
B. Jambo kuwa gumu
C. Kutofanikiwa
D. Kaa macho usiku kucha

**19.** Kiambishi ki kimetumiwa kuleta maana gani katika sentensi ifuatayo?
Wanacheka wakiimba
A. Kuonyesha kutegemeana kwa vitendo.
B. Kuonyesha vitendo viwili vinafanyika baada ya muda.
C. Kuonyesha vitendo viwili vinafanyika kimoja baada ya kingine.
D. Kuonyesha vitendo viwili vinafanyika wakati mmoja.

**20.** Chagua sentensi mwafaka inayounganisha hizi: Fatma alituzwa. Fatma hakufurahi.
A. Lau Fatma alituzwa hakufurahi
B. Fatma hakufurahi aghalabu alituzwa
C. Fatma hakufurahi licha ya kutuzwa
D. Maadamu Fatma hakufurahi alituzwa

**21.** Tunaitaje wakati kati ya saa sita na saa nane mchana?
A. Adhuhuri
B. Alasiri
C. Jua la utosi
D. Jua la matlai

**22.** Chagua usemi wa taarifa ufaao wa: "Nitasoma kwa bidii ili nifaulu", akasema.
A. Anasema kuwa anasoma kwa bidii ili afaulu
B. Alisema kuwa atasoma kwa bidii ili afaulu
C. Anasema kuwa angesoma kwa bidii ili afaulu
D. Alisema kuwa angesoma kwa bidii ili afaulu

**23.** Chagua hali ya kutendewa ya sentensi ifuatayo:
Mganga aliniganga kwa miti-shamba
A. Aliganguliwa na mganga kwa miti-shamba.
B. Niliganguliwa mganga kwa miti-shamba.
C. Niliganguliwa na mganga kwa miti-shamba.
D. Aliganguliwa mganga kwa miti-shamba.

**24.** Tegua kitendawili
Juu ya mlima kuna msitu mweusi
A. Chungu
B. Nywele
C. Mpingo
D. Makaa

**25.** Chagua kiwakilishi katika sentensi ifuatayo:
Niitie Juma nimtume, huyu amekataa kuenda.
A. Juma
B. Nimtume
C. Kuenda
D. Huyu

**26.** Ni maneno yapi ambayo ni vivumishi katika sentensi hii? Mbwa hatari waliwafukuza vijana wanne waliopita hapo.
A. vijana, wanne
B. hatari, wanne
C. waliwafukuza, vijana
D. waliopita, hapo.

**27.** Chagua kihusishi katika sentensi:
Kiboko mkali alimvamia mvuvi aliyesimama kando ya mto
A. kando ya
B. mkali
C. mvuvi
D. aliyesimama

**28.** Sentensi "Stella amekwenda kwao" ina maana mbili. Zichague
A. (i) Amekwenda alikozaliwa
(ii) Amekwenda mbali na kwao
B. (i) Amekwenda kwa mtu mwingine
(ii) Amekwenda mbali na kwao
C. (i) Amekwenda alikozaliwa
(ii) Amekwenda kwa watu wengine
D. (i) Amekwenda kwa watu wengine
(ii) Amekwenda mbali na kwao

**29.** Chagua sentensi yenye "na" ya kuonyesha mtendaji
A. Rosa ameandikiwa barua na Rahma
B. Akida na Anasa ni wanafunzi wazuri
C. Tamaa na ubinafsi ni chanzo cha uovu
D. Ninunulie matunda na mboga

**30.** Jina kutokana na kitenzi **hama** ni:
A. Amehama
B. Hamishwa
C. Hamia
D. Mahame

*Soma taarifa hii kisha ujibu maswali.*

Katika kijiji kimoja kijulikanacho kwa jina Makanyo, kuliondokea kijana mmoja ambaye Mungu alimtunukia bongo. Kijana huyu alijulikana kwa jina Tumaini. Darasani alikuwa hawezekani. Akasoma kwa bidii ya mchwa hadi akafika chuo kikuu na kuivunja rekodi kwa kukwangura alama nzuri ajabu. Baadaye akaoa mke kufu yake na kuwapata watoto ambao nao vilevile walizifuata nyayo za wazazi wao.

Jambo lililokuwa linaikera familia ya kina Tumaini lilikuwa ni ukosefu wa kuwajibika kwa ndugu. Kaka zake walikuwa wazembe na butu shuleni. Kila walipokanywa na kushauriwa kuwa wasome vyema kama ndugu yao Tumaini, walipuuza na kucheka, wakashindwa hata kuchungulia vile vidato vya sekondari vifunguavyo vijana macho na akili zaidi. Tabia zao zikazorota, wakawa wanapiga mtindi tu na kuzurura.

Ingawa tabia za ndugu hawa ziliendelea kuwa mbaya, Tumaini hakukata tamaa kabisa. Mara kwa mara aliwaita kuwashika sikio na kuwapa mawaidha. Alijitolea kuwalipia ada za kwenda kujisomea masomo ya ngumbaru ili angalau waweze kujishikiza katika sekta ya "Jua-Kali", lakini wapi! Walianza masomo na kuyaachia njiani.

Wazazi walipokaribia kuwapungia mikono wana wao humu duniani, waliwaita kwa pamoja na kutoa wasia na hata kuwapa urithi wa mashamba. Tumaini akawaambia ndugu zake kuwa kwa kuwa anao uwezo, yeye atawaachia hayo mashamba ili wayalime na kuweza kujiinua. Wazee wakafurahi kuona kuwa Tumaini alijali maslahi ya wadogo zake.

Baada ya vifo vya wazazi hao, wadogo hao hawakuchelea kuipiga mali shoka mara moja. Tumaini aliwaonya lakini aliambulia nunge. Maonyo hayo yote yaliingilia sikio moja na kutokea lile jingine, huku yakipurukia hewani.

Siku moja, ajali mbaya ya barabarani ikaamua kuyakatisha maisha mema ya Tumaini na mkewe. Huzuni iliwakumbatia wana wao lakini majirani na marafiki wakaingilia shughuli za mazishi na kuzimaliza. Wakaanza kuwatunza watoto ambao wakati huo walikuwa wakimalizia elimu ya shule ya msingi.

Nduguze Tumaini walikuwa wakidhani wamepata vya bwerere na kujiona wakifaidi mali ya Tumaini kama tu ile ya wazazi. Hata hivyo, juhudi si pato, waliyoyataka hayakuwa. Marafiki wa Tumaini waliyatilia guu matendo ya ndugu hawa ambao walikuwa wameanza kuinyemelea mali ya Tumaini. Walijaribu kwa udi na uvumba kuzuia dhuluma hii na walipoona mambo yatachacha wakawasaidia watoto kwenda katika korti ya watoto kutetea haki zao. Ami za watoto hawa wakashtakiwa kwa madai ya jaribio la unyang'anyi wa urithi. Uzuri ukawa Tumaini na mkewe nao walikuwa wameandikisha urithi wa watoto wao na kumwachia wakili. Wakili aliwaonyesha nduguze Tumaini hati hizo, wakawa hawajui pa kuziweka nyuso zao. Wakajua kuwa watoto nao wana haki za kurithi. Pia walielewa kwamba kusoma ni kuzuri. Kama wangalisoma vyema wangalikuwa na vyao, lakini walibaki kuwa hohehahe wasio na mbele wala nyuma. Wakawa wanategemea cha ndugu ambacho hakikuwasitiri.

**31.** Tumaini alithibitisha werevu wake kwa
- A. kupita mitihani yote, kuonya ndugu, kutii wazazi, kuacha urithi wake
- B. kupita mitihani yote, kupenda majirani, kuwaachia wanawe urithi chini ya wakili
- C. kupita mitihani yote, kuonya ndugu, kuwaachia wanawe urithi chini ya wakili
- D. kupita mitihani yote, kupenda ndugu, kuwaachia urithi chini ya wakili

**32.** Wazazi wa Tumaini walikuwa na busara kwani
- A. waliwapa wasia wana wao wamtii Tumaini
- B. waliwaachia wana wao urithi
- C. walikuwa na maonyo mengi
- D. waliwaonya wana wao wakasikia

**33.** Ndugu wa Tumaini waliposhauriwa wasome walicheka kwa sababu
- A. Tumaini hakuwa tajiri ijapokuwa alisoma
- B. walitarajia kufaidi mali ya ndugu yao
- C. hawakuona haja ya masomo
- D. walishindwa kuendelea na masomo

**34.** Nduguze Tumaini
- A. waliachia masomo shule za msingi
- B. walisomea kazi za ufundi
- C. walifundishwa kazi za jua kali wakashindwa
- D. walisoma ngumbaru wakakosa kupata kazi

**35.** Maana ya <u>mke kufu yake</u> ni
- A. mke wa jamii yake
- B. mke aliyelingana naye
- C. mke wa kijiji chake
- D. mke aliyesoma naye

**36.** Baada ya vifo vya wazazi wao, nduguze Tumaini,
- A. walidhani watafaidi mali
- B. waligawiwa mali wengine wakaifuja
- C. walimnyima Tumaini urithi wote
- D. walianza kuifuja mali mara moja

**37.** <u>"Huzuni iliwakumba wana wao lakini majirani na marafiki wakaingilia shughuli za mazishi na kuzimaliza".</u> Hali ya huu msaada inaweza kuelezewa kwa methali:
- A. Damu ni nzito kuliko maji
- B. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki
- C. Kenda ni bora kuliko kumi nenda rudi
- D. Ndugu mui heri kuwa naye

**38.** Haki za watoto zilitimizwa kwa
- A. kusomeshwa, kuonywa, kusaidiwa, kuishi na ndugu wakiwa mayatima
- B. kulindiwa urithi wao na ndugu, kugawiwa urithi na kusaidiwa na majirani
- C. kusomeshwa, kusaidiwa walipofiwa, kupewa urithi na kuelekezwa kushtaki maonevu
- D. kutomruhusu yeyote kuwanyang'anya mali, kuelekezwa kwa mashtaka na kuruhusiwa kuuza mali

**39.** Kulingana na kifungu, <u>kuipiga mali shoka</u> ni:
- A. kutumia mali vibaya
- B. kugawanya mali yote
- C. kuhifadhi mali yote
- D. kupiga mali bei

**40.** Neno <u>hakikuwasitiri</u> kama lilivyotumika katika kifungu linamaanisha
- A. hakikuwafunikia aibu
- B. hakikuwakamilisha
- C. hakikuwatamanisha
- D. hakikuwatosheleza

*Soma taarifa hii kisha ujibu maswali.*

Usafiri katika nchi nyingi za Kiafrika ni tatizo sugu. Baadhi ya watu hutembea kwa muda mrefu kwa miguu kwa kuukosa usafiri wa haraka. Wengine hupanda hata ngamia ili wapige hatua. Pia, punda hutumiwa kusafirisha mizigo. Kwa wale waliodiriki kujinunulia magari,,muda haupiti kabla ya ukarabati kuhitajika. Mamilioni ya magari ya aina hiyo huwa tu ni ya kubebewa nyundo na parafujo kila wakati. Hali hii imezidishwa na barabara ambazo hazijatiwa lami au hata zikiwa zimetiwa, hupachikwa kiholela tu. Mashimo barabarani yanaharibu magurudumu na hata magari yenyewe. Isitoshe, ukata katika jamii unachangia uhaba wa magari mazuri na hata ubovu wa hayo machache. Hii ni kwa sababu watu hawana ngwenje za kununulia vipuri vifaavyo au kujinunulia magari mapya.

Wengine hujikidhia mahitaji yao ya usafiri kwa kutumia baiskeli. Hizi zina nafuu kifedha kuliko magari, lakini haziwezi kubeba mizigo mingi na mizito. Wachache sana hutumia eropleni na meli ambapo wengi huweza kuyatumia magari moshi. Magari moshi hubeba watu na vitu kwa wingi. Gharama za ukarabati wa reli, mabehewa ya magari hayo na injini zao, zimesababisha ongezeko kubwa la nauli katika miaka ya hivi karibuni. Watu wengi wanashindwa kuulipia usafiri huu. Baadhi yao huyadandiadandia magari hayo hadi paani mwa mabehewa na mabogi ili tu wakwepe kulipa nauli. Mtindo huu hautatizi tu shirika la reli bali huzua hatari kwa wasafiri. Baadhi ya wadandiaji huporomoka na kujivunjia viungo, jambo ambalo huongeza idadi ya walemavu bure bilashi.

Matatu na mabasi ni aina ya uchukuzi ambao ni maarufu nchini Kenya. Uchukuzi huu umekuwa ukiwafaa watu wengi sana kwa miaka na dahari, hasa wale wa kima cha chini na cha wastani. Jambo linalowaudhi abiria zaidi ni ukosefu wa kudhibiti mambo mengi yanayohusiana na aina hiyo ya usafiri. Mathalani, kudhibiti mwendo wa magari hayo, tabia za utingo na madereva na kujaza watu garini kama makopa. Zaidi ya hayo, imekuwa ni shida kuzidhibiti tabia za wale wapendao kurambishwa asali katika sekta hii.

Hivi majuzi, waziri wa usafiri na mawasiliano alifanya juu chini akaibuka na mikakati kabambe ya kuondoa udhia mwingi katika sekta ya usafiri. Aliwataka wenye magari kuweka vidhibiti mwendo, abiria kuitumia mikanda ya usalama, utingo na madereva kuvaa sare na magari kutobeba abiria kupita kiasi. Kwa kuwa wenye magari wengi hawakuweza kutimiza masharti hayo kwa muda uliowekwa, ilibidi magari mengi yasitumike kwa muda.

Abiria ambao walikuwa wamechoshwa na vituko barabarani walipiga moyo konde na kujisemea, "Si hoja, hata kama itabidi tutembee kwa miguu kwa muda ni sawa, mradi tupate suluhisho la kudumu".

Kulingana na matokeo ya uchunguzi uliofanywa muda mfupi uliopita, imegunduliwa kuwa tayari ajali zimepungua, usafiri umekuwa wa utulivu na nidhamu ya utingo na madereva imeimarika. Zogo la "kama hutaki kubinywa nunua lako" limekwisha kabisa.

41. Mwandishi amezitaja aina zifuatazo za usafiri:
A. miguu, wanyama, udandiaji, gari moshi.
B. gari moshi, gari, miguu, baiskeli.
C. wanyama, pikipiki, udandiaji, ndege.
D. miguu, baiskeli, ndege, pikipiki.

42. Kulingana na kifungu watu hudandia magari ya moshi kwa sababu
A. usafiri ni wa bei nafuu
B. wanataka kuepuka udhia wa usafiri
C. usafiri wa magari ni ghali
D. wanataka kuepuka kulipa nauli

43. Kifungu kinasema kuwa njia ya usafiri inayotumika sana ni
A. barabara
B. eropleni
C. baiskeli
D. gari moshi

44. Mambo yanayochangia katika kuzorotesha uchukuzi ni
A. umaskini, njia mbaya za uchukuzi na ukosefu wa vidhibiti
B. ukosefu wa lami, kudandia magari na kutokarabati magari
C. uhaba wa magari, ukosefu wa kuwadhibiti abiria, ukwepaji wa nauli
D. mashimo barabarani, ukarabati na uendeshaji kasi

45. Magari ya kubebewa nyundo na parafujo kila wakati ni magari
A. mabovu
B. mapya
C. ya uchukuzi
D. ya wakarabati

46. Kujivunjia viungo kwa mujibu wa kifungu ni
A. kuvunja viungo bila usaidizi
B. kujisababishia kuvunjika kwa viungo
C. kuvunja viungo bila sababu
D. kujivunjia viungo kwa makusudi

47. Suluhisho kuu la usafiri wa barabarani ni:
A. Kuwazungumzia polisi, madereva na wenye magari
B. Kuwazungumzia na kuwadhibiti wasafiri
C. Kuwafuta wasiotimiza masharti
D. Kudhibiti kila kitu kibaya kinachohusu usafiri

48. Abiria walisema . . . "si hoja, hata kama itatubidi tutembee . . ." kwa sababu
A. walikuwa wamechoka kulipa nauli za juu na kudandia
B. walikuwa wamechoshwa na magari ya moshi
C. walikuwa wakitaka mikanda ya usafiri na vidhibiti mwendo
D. walikuwa wameudhishwa na shida za usafiri

49. Mabadiliko yaliyowekwa katika sekta ya usafiri hivi majuzi yamesababisha
A. usafiri kuwa wa utulivu, utingo kuwa nadhifu zaidi
B. kuimarika kwa nidhamu ya utingo na madereva na zogo kupungua
C. kupungua kwa ajali, nidhamu ya utingo na madereva kuimarika, usafiri kuwa wa utulivu
D. kuimarika kwa vidhibiti mwendo na nidhamu ya utingo na madereva

50. Maana ya wapendao kurambishwa asali ni
A. wapendao kula vitamu
B. wapendao kula hongo
C. wapendao anasa nyingi
D. wapendao vya bure